

... nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu
ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.

Wafilipi 3:14



Kibondo Anglican Training Centre





Kibondo Anglican Training Centre inawakaribisha watu wa umri ndogo, watayarishwe vema kwa majukumu mbalimbali ndani ya makanisa yao.

Huduma hiyo inaweza kufanywa kwa kujitolea, au kama mfanya kazi kamili wa kanisa. Shabaha ya Kibondo Trainig Centre ni kuwapatia elimu ya msingi kwa ajili ya huduma hizo za kuwalea waumini kiroho na kiimani wapate kukua.



Mafunzo ya Theologia

Kozi ya msingi ya miezi 3
inafundishwa Januari hadi Pasaka

Kozi ya kuendeleza ya miezi 6
inafundishwa Pasaka hadi Oktoba

Kozi ya kukamilisha ya miezi 9
inafundishwa Januari hadi Oktoba

Kozi za kuendeleza za kawaida

Kozi kwa ajili ya walimu wa shule ya jumapili (*Sunday school Teachers*)
inafundishwa katika kosi mbili: Machi hadi Aprili na Septemba hadi Oktoba

Kozi za pekee kwa ajili ya Wainjilisti na Wachungaji

Semina kwa watu wenye ndoa na kwa wanawake

Mafunzo kwa ajili ya viongozi wa *(wazee wa kanisa)*

makaniza Mikutano ya vijana

Ada za Kozi na gharama kwa malazi na chakula:

		2019
Kozi ya msingi ya miezi 3	TSH	160
Kozi ya kuendeleza ya miezi 6	TSH	310
Kozi ya kukamilisha ya miezi 9	TSH	460
Kozi kwa Sunday School	TSH	90
Kozi za kuendeleza za kawaida kwa kila siku	TSH	00
Malazi na chakula kwa kila siku	TSH	15

Kibondo Anglican Training Centre bado haijawa na uwezo wa kujitegemea kifedha – kama kawaida kwenye Shule za Bibilia. Kwanza kwa ajili ya kuinua majengo ya kufaa, ndipo kozi mbalimbali kwa ajili ya Wainjilisti na Wachungaji pia zinategemea matoleo ya watu wa Mungu. Tungefurahi kama wewe nawe ukituunga mkono kwa changizo lako kwa ajili ya kuendeleza kituo chetu.

ing Centre
ERD -



privat, Noell Kaew



Kuitwa kwa huduma ya Mungu !

Samweli Isaka* anaishi vijijini, sehemu za magharibi ya Tanzania. Anayo ndoa na Sara, nao wana watoto wawili, mvlana na msichana. Mama ana mimba ya mtoto wa tatu. Yeye ni mshiriki wa Kanisa Anglikana katika kijiji cha-ke, anaongoza ibada za watoto (sunday school), na pia anahibiri karibu kila Jumapili. Zaidi ya hapo anawahudu-mia wazeena wagonjwa akiwatembelea kwa taratibu.



Kanisa lake si kubwa zaidi. Jumapili watu kama 50 wanahuduhuria ibada, bila kuhesabu watoto. Kuwa na Mchungaji wa kanisa bado hawajiwezi kifedha. Karibu washiriki wote hawana pato kamili. Kila mmoja anayo kipande cha shamba analotegemea kwa kuvuka mwaka. Hata hivyo kuna mwalimu mmoja kati yao. Huyu tu anayo mshahara kamili. lakini hata yeye anategemea mavuno ya shamba lake, ili aweze kuishi sawasawa. Hata hivyo kila Jumapili wanakusanya sadaka, inayo-saidia kulipa posho kwa Mwinjilisti (Msaidizi wa Mchungaji).

Mwaka uliopita wazee wa kanisa waliamua, wamtume Samweli masomoni Kibondo. Kituoni ajipatie elimu na ujuzi wa kufaa kwa huduma zake kama Mwinjilisti. Kosi ya msingi ya miezi 3 na kosi ya kuongeza miezi 6 amekwisha kumaliza vizuri. Sasa kanisa linachangia kwa kumlipia ada ya kosi ya kumaliza ya miezi 9. Ndio atategemewa kurudi hudumani mwake kama Mwinjilisti kamili. Hata hivyo posho yake haitakuwa kubwa zaidi. Mwinjilisti hupokea kati ya TShs.13.000 hadi 52.000. Kufanya kazi kama

Mchungaji, bila shaka hataweza kabisa, maana hapo ingempasa kuoma miaka 3 kwenye Chuo cha Biblia ya Kasulu.

Wanahitajika wanaume wengi kama Samweli, watu wanaotenda huduma yao kwa uaminifu. Ila inapaswa watayarishew vema: Uwezo wa kufafanua Bibliavizuri, uwezo wa kuhubiri, kuwalea watu kiroho, na mengine zaidi ya hayo.

*Habari hiyo imetungwa, lakini hali hiyo ndiyo mais-ha ya Mwinjilisti katika Kanisa Anglikana.

